*Enyi mlioamini, muitikieni Allah s.w na Mtume wake anapokuiteni katika yale yatakakupeni uhai……*

# Khilafah

## ndio suluhisho

SHAABAN 1438 A.H. ··· MEI 2017··· TOLEO: 57




# BILA YA KHILAFAH

1.SHAABAN MWEZI WA MABADILIKO: 2.MAKABURI YA HALAIKI CONGO UDHAIFU WA UN: 3.MEI MOSI SIKU YA HADAA KWA WAFANYAKAZI: 4.KUFAIDIKA NA RASILIMALI KWAHITAJI MFUMO MBADALA: 5.BILA KHILAFAH DAMU YA WAISLAM NI DAMU YA MAJARIBIO YA SILAHA: 6.SWALI KWA AMIR: ZAKAT YA DENI: 7. AHLUL SUNNAH : SUNNAH KUELEKEANA NA BIDAA; SEHEMU YA TATU

# DONDOO ZA HABARI

## // UFILIPINO YAPUNGUZA MNO UCHIMBAJI WA MADINI



Serikali ya Ufilipino imefuta mikataba 75 ya uchimbaji madini na kufunga zaidi ya 50% ya migodi yote. Ikiwa ni nchi inayoongoza kwa uzalishaji wa madini ya Nickel, Ufilipino imepata madhara makubwa kwa sekta hii kuliko faida.

Hii ni baada ya raia kuanza kukereka na madhara ya uchimbaji haliiliyoanza kuashiria vurugu. Wanaharakati wa mazingira akiwemo Regina Lopez wameweka wazi kwa kuwalaumu wawekezaji mabepari wa nje kwamba "mnau vyanzo vya maji, mnadhuru maisha, mnaua mito, kilimo na maji ya kunywa na haribu. Ni miradi inayo "tubaka".

Hali hii ndivyo ilivyo duniani kote hususan kwenye 'wawekezaji' ambapo raia huendelea kuwa masikini huku mali ikiporwa na wachache, mabepari na watawala.

## // UHUNI WA KIDEMOKRASIA WAMPA USHIND ERDOGAN UTURUKI

Rais wa Uturuki Tayyip Recep Erdogan ameweza kupitisha mawazo yake ya 'mabadiliko' ya katiba kupitia kura ya maoni kwa kuungwa mkono na 51.4% ya kura zilizopigwa. Kuelekea upigaji kurahuu Erdogan alishajenga mazingira ya kuwatisha raia na kupora maamuzi yao. Akiwa anajua ukibaraka wake unafahamika na kuchukiwa na raia alianza na kuweka mazingira ya matamko ya hali ya hatari na kudhibiti vyombo vya habari. Lakini bado raia wamemdhihirishia kwamba ataendelea kutawala miili yao, kwa mtutu lakini hawakubali ubepari na demokrasia anayo simamia.




Mabadiliko yanalenga kumpa Rais nafasi juu ya sheria na kuondoa uwezo wa bunge kumuhesabu.

Ikiwa ni kura ya kuimarisha ubwanaukibaraka wake kwa Marekani, amepongezwa na Rais bwa Marekani Donald Trump. Hii nikwasababu ninafasi kwao kuendeleza mauaji ya waislam Syria na ukaliaji ardhi za waislam mashariki ya kati.

## PAMOJA NA KUUONDOSHA UKABURU, UBAGUZI NA UONEVU WAENDELEA AFRICA KUSINI

Familia ya Mandela yaanza kuichoka ANC baada ya baadhi ya wanafamilia kutamka hadharani kutokukiunga mkono chama hicho. Ndileka Mandela, mjukuu wa Nelson Mandela na mfuasi mahiri wa ANC amebainisha. Mivutano na misukumo ya kumtaka Rais Jacob Zuma ajiuzulu imeendelea kupamba habari za dunia ikiashiria kuanguka kwa chama cha ANC. Kutawala kwa ANC ilikuwa ni baada ya kuuondoa utawala wa kikaburu uliokuwa wa kibaguzi na ufujaji rasilimali za ummah.



Zuma ana shutumiwa kwa ufujaji wa mali za ummah. Akiwa miongoni mwa wapigania Usawa na kuuondoa ukaburu, leo hii ndiye anafanya ya makaburu ikimaanisha yalikuwa mabadiliko ya watu na vyama lakini hali ipo vilevile kwakuwa ni zao la kimfumo. Na ni tawala za kimaslahi kwani hata familia za watawala hufaidika kwa nyadhifa za wazee wao ndipo sasa wanafamilia ya Mandela wanahisi kupoteza.

## ZIARA YA PAPA MISRI NA KUIMARIKA DINI MSETO

Papa Francis, kiongozi wa kilimwengu wa kanisa dola la Katoliki amefanya ziara ya saa 27 nchini Misri siku ya tarehe 28/4/2017. Akipokelewa kwa heshima zote za kijeshi alikutana na kuzungumza na Rais Abdel Fattah al-Sisi ambaye ni Rais wa kwanza wa Misri kuingia kanisani.



Pia alitembelea chuo kikuu cha waislam cha Al-Azhar ambapo alikutana na Muft mkuu Ahmed al-Tayyeb na kufanya mazungumzo. Ameelezea dhamira ya ziara yake ni kushajiisha kudumisha Umoja na Undugu. Alipata nafasi ya kuhutubia ummah alipokuwa katika chuo cha Al-Azhar.




Ziara hii nikatika juhudi 'zake' kama wakala mkuu wa kusambaza na kuimarisha Dini mseto, fikra haram na hatari kwa ummah wa waislam kwani inalenga kuiweka Aqidah ya kiislam katika mizani sawa au duni kwa imani nyingine za kilimwengukama ukristo, ubudha na uyahudi.

Al-Azhar kimekuwa mshirika mkubwa na wa asili tangu kuasisiwa fikra hii ambapo katika mikutano ya awali mmoja ulifanyika katika chuo hiki kikongwe mnamo mwaka 1932 chini ya ujumbe kutoka Ufaransa.

# Tahariri

## SHAABAN NI MWEZI WA MABADILIKO NA USHINDI KWA WAISLAMU .



Mwezi wa Shaaban 1438 H umewadia sawa na tarehe 27Aprili 2017 M . Mwezi huu ni mwezi wa mapambano baina ya haki na batili pale hujma kubwa ilipofanywa na muungano wa majeshi ya Ulaya na kanisa dhidi ya ardhi tukufu ya Jerusalem (Baitil maqdis) .

Baada ya uvamizi wa majeshi ya Ulaya na kanisa chini ya bango lao la vita vya msalaba(crusaders) Julai 15 mwaka 1099 M sawa na Shaaban 13 mwaka 492 H. Waislamu hawakurudi nyuma na kukata tamaa bali waliendelea na mapambano dhidi ya watu wa msalaba kwa kipindi kisichopunguwa miaka mia mbili(200) kuikomboa ardhi tukufu ndani ya Palestine kwa mihula saba (7) bila ya kukata tamaa na hatimaye kupata ushindi dhidi Wamongoli na watu wa msalaba kwa vipindi tofauti chini ya Majemadari kadhaa wa kiislamu mwaka 1268 M. https://en.wikipedia.org/wiki/Siege_of_Jerusalem_(1099

Kilichowasukuma waislamu kuwa mashujaa na kukabiliana na vitimbi na uvamizi wa watu wa msalaba ni kukinai na Aqeeda yao na kuwa chini ya viongozi walio waongoza kukabiliana na changamoto zote zilizojitokeza. Wao walisha ahidiwa na Allah kuwa ndio wakuitawala dunia na watakuwa juu ya makafiri kwa sharti kuwa wawe wameamini kwa yote yatokanayo na Mola wao Mlezi . Allah anasema :

وَلاَ تَهِنُوا وَلاَ تَحْزَنُوا وَأَنْتُمْ الأَعْلَوْنَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ (آل عمران: 139

*'Na msilegee(msiregee) wala msihuzunike , maana nyinyi ni wajuu ikiwa mnaamini kweli.'*

Ahadi hii wakaiamini na kuifanyia kazi kwa vitendo na juhudi na ikaufanya mujtamaa wenye kutisha nguvu za makafiri chini ya ngao zao yaani Majemedari wa kiislamu. Kwa hivyo Mwezi wa Shaaban utuhimize wasilamu kufanya ibada kwa wingi lakini utusukume kufuata nyayo za watu wema walio tangulia , wa kufanya harakati na mapambano ya kifikra na kisiasa kuzikomboa ardhi tukufu na maeneo mengine yenye kukaliwa na makafiri kwa mabavu.

Yanayotokea hivi sasa ulimwenguni ya Vinara wa mfumo wa demokrasia ambao ni Marekani na madola ya Ulaya wakishirikiana na Wazayoni (Israel) kukalia ardhi tukufu ya Palestine , tubebe kama ni changamoto kwetu na tujipange kupambana kifikra na kisiasa hadi tuwango'we waondoke katika ardhi hizo. Damu zinazomwagwa za waislamu wenzetu pembe zote za dunia tuone ni damu zetu .Mateso yao ni mateso yetu na yaibue hisia ya kuwa tayari kupambana nao kifikra na kisiasa .Inatosha yanayotokea Palestine, Kashmir, Bhurma, Bangladesh,Bosnia, Xijiang(China),Afghanistan,Misri,Iraq, Syria nk.kutusukuma waislamu kufanya juhudi ya kuunusuru umma chini ya Majemedari wa kiislamu wanao fahamu uislamu wao na kuiamini aqeeda yao .

Jee yawezekana kuyatimiza hayo kwa hali tuliyonayo ?.Inawezekana madamu ile ahadi ya Allah ipo kwa ajili yetu . Jambo muhimu tuamini kuwa sisi waumini ndio warithi wa ardhi hii .Mtume saaw ametuonyesha kifikra na vitendo juu ya kukabiliana na hali tuliyo nayo kwa kufanya daawa kifikra na kisiasa kufanya mabadiliko ya kuondoa mfumo batili wa Maqureish na pahala kutabikisha mfumo wa uislam kwa kuasisi dola ya kiislamu Madina na akasema baada ya kufa yeye tuwatawalishe Makhalifah wasimamie dola ya kiislamu /Khilafah ili watungoze kupata ushindi dhidi ya maadui zetu.

Dunia hivi sasa hata wasiokuwa waislamu wamechoshwa na maovu ya mfumo wa Demokrasia na viongozi wake kwa kukithirisha dhiki kwa wanaadamu walio wengi.

Tukumbuke kuwa sasa ni zaidi miaka themanini tu (80)tokea ianguke Khilafah , Uturuki mwaka 1924 M. Huo ni muda mchache ukilinganisha na miaka mbili (200) ya mpambano baina ya waislamu na wavamizi wa msalaba. Ndugu zetu wa zama hizo hawakukata tamaa wakisukumwa na ahadi ya Allah swt. Kwanini sisi wa zama hizi tuchoke upesi na kukata tamaa.?Ahadi ya Allah ni yetu sote .Waislamu tutumie mwezi wa Shaaban kama fursa adhim kwetu kuzidisha daawah na juhudi kuukomboa ulimwengu na idhlali ya mfumo wa demokrasia .

***Bila ya khilafah ni utumwa na dhulma.***

**Mharir**
**Jarida la Khilafah**

**Shaban, 1438AH, Mei 2017AD**




# MAKABURI YA HALAIKI NCHINI KONGO NI DHIHIRISHO LA UOZO WA VIKOSI VYA KULINDA AMANI

Hivi karibuni kumegunduliwa kwa kuwep makaburi mengi ya halaiki yenye kukusanya idadi kubwa ya miili ya wafu yapatao takribani 40 kwa mujibu wa Ripoti ya umoja wa mataifa iliyotolewa siku ya Jumatano 19-04-2017 iliyodai kugunduliwa makaburi hayo na vikosi vyake vya kiusalama. www.bbcswahili.com.

Makaburi hayo yanayodaiwa kutokana na mapigano ya hivi karibuni kati ya jeshi la nchi hiyo na waasi wanaojiita kundi la Kamuina Nsapu na kusababisha uharibifu mkubwa wa mji na hata makaazi ya watu pamoja na shughuli za kimaisha kwa ujumla.
Makaburi haya si mara ya kwanza kugundulika Kongo bali ni kila mwaka takriban hivi sasa tokea kuanza kwa mapigano nchini humo hugundulika makumi ya makaburi kama haya ya kisheheni idadi kubwa ya miili ya wafu. Haitoshi kwa kongo tu suala hili limekua likijitokeza takribani ulimwenguni kote kwa kila nchi inayokabiliwa na machafuko khususan ya wenyewe kwa wenye yaani baina ya vikosi vya serikali na wananchi wake, ama makundi ya raia wenyewe kwa wenyewe kwa kubambikiwa jina la waasi.
Kama ilivyo kwa Kongo nchi za Syria , Yemen na hata Afrika ya kati ni wahanga wakubwa wa kadhia hizi kwa miaka kadhaa hivi sasa, cha kushangaza na cha kutia aibu vile vikosi vinavyopelekwa katika nchi hizo kwa ajili ya kulinda kile kinachoitwa amani vikishuhudia mauaji hayo pasina kuchukua jitahada zozote kuzuia ama kuhifadhi raia ambao ndio wahanga wakubwa wa mauaji hayo na wakati mwingine vikishutumiwa kuhusika kuuwa raia waliosema wanawalinda.

Kilichotokea Afrika ya kati kwa wanajeshi wa Ufaransa kinakaribiana ama kufanana moja kwa moja na kile kilicho wakumba mashahidi waislam wa bosnia. Vikosi vya Ufaransa viliwanyanganya kwa nguvu silaha wanamgambo wa waislam wa seleka tahamaki tu mbele ya macho yao muda huo huo kuwaachia huru wanamgambo wa anti balaka wakiristo wakawavamia na kuwauwa kiurahisi kana kwamba wanachinja kuku kwa ajili ya sherehe zao za kimila.
Vikosi vile vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa vikiongozwa na Ufaransa vikajikosha kuwa wao hawakwenda pale kwa ajili ya vita bali ni kwa aijili ya kulinda amani tu. Ni amani gani waliyokwenda kulinda vikosi hivi ? kiasi cha kuachia watu wa kiuana mbele ya macho yao na wao kufunga mikono yao wasichukue hatua yoyote ile kana kwamba wameagiza kutekelezwa unyama huo.
Vikosi hivi vimekua havina msaada wowote si kwa kulinda hio inayo itwa amani kwa raia wanyonge madhlum wanchi zile ambao ndio wahanga wakubwa wa mauaji haya katika pembe zote za ulimwengu huu. bali kazi yao kubwa ni ubakaji na wizi kwa mali za raia hao kama vile ilivyotokea nchini Somalia mwaka 2016.
"Mkuu wa Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia maswala ya Haki za Binadamu Zeid Ra'ad Al Hussein, mwaka uliopita, alisema kuwa uchunguzi wa watalaam wake ulibaini kuwa wanawake 18 walikuwa wamebakwa na wanajeshi wa Uganda katika eneo la Obo" umoja wa mataifa. ww.d.w/kiswhili.com.

Ripoti kama hizi na nyingi nyenginezo zinazotolewa na umoja wa mataifa wenyewe kama ile ya wanajeshi wa Ufaransa kufanya vitendo hivi hivi vya kinyama vya ubakaji na kunajisi watoto wadogo nchini Afrika ya kati ni dhahiri kuwa vikosi hivi vya kishenzi visivyopaswa hata kulinda wanyama pori katika nchi zao.
Ikiwa katika hali hii ya vita na simanzi na kutawala kwa milio ya risasi kila wakati katika nchi hizo wao ndo huifanya ni fursa ya kufanya jinai zao, hali ikoje kwa vikosi hivi vinapokua katika makambi nchini mwao wanavyoamiliana na raia wanaopingana na sera za serikali zao zinazo walipa mishahara?

Yote haya si ajabu kwa mfumo huu uliooza wa kidemokrasia unaotawala ulimwengu leo kwa njia yake yake mpya ya propaganda zisizo kwisha kila uchao ili kujipa muda wa kupumua katika kuendelea kuutawala ulimwengu kwani kwa hakika muda wake umeshafikia ukingoni na bado masaa machache tu kuanguka na kuingia katika kuburi la halaiki la sahau kama lililo ukumba mfumo wa kikoministi.
Uislam pekee ndio wenye uwezo wa kuhifadhi amani ya ulimwengu huu kama vile alivyosema Allah taala kupitia kitabu chake kitukufu kuwa ( hapa ije aya ya amani itawapata wanaofuata muongozo)
**Na: SULEIMAN JAULA.**




# MEI MOSI: Siku ya hadaa kwa wafanyakazi

Kila tarehe mosi mwezi wa mei kwa sehemu kubwa ya dunia ni siku iliyopewa jina la 'siku ya wafanyakazi'. Kama ilivyo sherehe na maadhimisho mengine ya kupangwa kiserikali katika kuwahadaa watu hii nayo ni maalum kwa wafanyakazi. Mfanyakazi ni mtu yeyote mwenye jukumu la kuhakikisha jambo fulani maalum linafanyika nayeye akipata manufaa kwa utekelezaji huo hususan kwa kuajiriwa.

Msingi mkuu wa mfanyakazi ni uwezo wa kulitekeleza jukumu husika. Uwezo huu ni wa kinyenzo; yaani akili na zana. Mtu huy hujengeka kiakili (maarifa na ujuzi) na kuwa na zana (mashine na vifaa vingine) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji huo. Vitu hivi kupatikana kwa mtu yeyote ni jukumu la serikali, moja kwamoja kwa kumpatia elimu muafaka na kumjengea fursa za kutumia elimu hiyo. Au isiwe moja kwa moja kwa kujenga mazingira rafiki kwa mtu kupata vitendea kazi baada ya kupatiwa elimu na serikali. Ili ifikie wakati mtu huyu ajijengee maisha yake na kujenga taifa lake.

Historia imeonesha namna watawala kote katika ulimwengu wa kidemokrasia wanavyo wafanya wafanyakazi wao kuwa daraja la watawala kufikia 'ndoto' zao katika hali ambayo wao wafanyakazi huwa ni wafanywakazi na ndoto zao hutoweka na kuwa hohehahe. Mfano mzuri ni historia ya asili ya siku ya wafanyakazi duniani, mei mosi kwa sehemu kubwa ya dunia.

Ilikuwa ni baada ya wafanyakazi kuamua kupaza sauti zao dhidi ya dhulma, uonevu na udhalilishaji uliofanywa juu yao na waajiri wao, zikiwemo serikali zao ambao ndiwo Watawala /waajiri waliweka zaidi ya masaa 12 kwa siku kufanya kazi na siku sita kwa juma. Wakahamasishana kupitia wapinzani wamfumo, wajamaa. Kama Karl Max (baba wa Ujamaa) alivyosema kuudhihaki Ubepari *kwa kurefusha muda wakufanyakazi, sio kwamba tu Ubepari una maliza nguvukazi ya watu kwa kanuni zake (mbove) na mazingira yake (mabovu) bali pia hupelekea uzalishaji usio wa kiwango na vifo vya wafanyakazi*. Ni katika kuonesha hisia zao, wafanyakazi waliandamana kwa amani nchini Marekani 4/5/1886 ambapo kulitokea mlipuko (leo hii ungekuwa ugaidi) na waandamanaji wengi walikufa. Ndipo ikachaguliwa na 'wanaharakati' wa kijamaa siku ya mei mosi kuwa ya kumbukumbu na ya muendelezo wa kudai haki. Tangu wakati huo hadi hivisasa haki hazija na hazita patikana kwa mfumo huu.

Maslahi na haki zinazo daiwa imekuwa kama kusubiria Ibilisi kusilimu. Kwani bila unyonyaji, ukandamizaji na udhalilishaji hakuna ubepari. Hivyo ili uendelee kuwepomfumo huu lazima kero za wafanyakazi ziwe sehemu ya maisha yao.

**Wataendelea kulipwa mishahara duni, tena ambayo ipo chini hata ya makubaliano ya kisheria zao, duni kiasi cha kutokutosha katika maisha ya kawaida.**

Mshahara mdogo wanakukata eti unawekewa pensheni utakapo staafu ukiwa na miaka khamsini upewe ikusaidie, wakati huohuo utabiri wao nikwamba muda wakuishi ni miaka 53. Yaani wanauhakika katika waajiriwa 100, labda 40 tu ndiwo wata staafu. Na ukisha staafu unaweza kumaliza miaka kadha hujalipwa, yaani wana jihakikishia katika wale 40 labda 20 tu ndiwo wata pokea posho yao. Lakini ikusaidie nini ukiwa umechoka kiakili na mwili, umesha haribu familia kwa kukosa uwezo na kuwasomesha shule za hovyo. Kodi katika mshahara inakufanya uwe mtoa kodi mkubwa kuliko mfanya biashara wa mamilioni. Mfano kwa mshahara wako wa TSh 1,500,000/= kwa wachache sana waliofikia hapo, unakatwa 309,000/= kodi, 75,000/= pensheni, bima na vyama vya wafanyakazi. Kodi tu unakatwa 3,715,200/= kwa mwaka wakati kwa muda huo mfanyabiashara mwenye kipato kuanzia mil 14 hutozwa kodi isiyozidi laki 3 kwa mwaka na anaruhusiwa kulipa.kwa awamu hadi 4. Na ukiwa unadaiwa na bodi ya mikopo utabakia na takribani TSh.900,000/= za kuendeshea maisha yako ukiwa katika nyumba ya kupanga, nauli na chakula kazini, familia, afya na elimu kwa kununua.


Ukijitutumua kuwa na njia nyingine ya uzalishaji, mfano kilimo, bado soko hakuna na likiwepo kodi za ajabu zinakuandama.

Leo umeanzishiwa vyama vya wafanyakazi ili iwe rahisi kukudhibiti japo unaona vinakusaidia.

Itakapo simama Serikali ya kiislam (Khilafah) duniani kama ilivyokuwa siku za nyuma suala la wafanyakazi ni wajibu wa serikali, kuwaandaa na kuwawezesha watu wake kufanya kazi.

***Inaendelea Uk 7***

# KUNUFAIKA NA RASILIMALI KUNAHITAJI MFUMO MBADALA DUNIANI



Mnamo tarehe 8 aprili gazeti la THE GUARDIAN nchini Tanzania liliandika taarifa kwamba ndege zenye mithili kama meli (airships) zitasafirisha gesi kutoka Tanzania na kupeleka ughaibuni/nchi za nje. Kampuni inayoitwa Helium One ya nchini Norway ndiyo iliyo gundua hazina kubwa ya gesi hiyo Tanzania. Katika taarifa ambayo ilinukuliwa na gazeti hilo ilisema kwamba kampuni hiyo imeingia mkataba na kampuni ya Hybrid Enterprises kwa ajili ya kutumia ndege hizo ambazo zitasafirisha gesi hiyo mpaka kwenda katika nchi za ughaibuni.

Kampuni hiyo imekaririwa kusema kwamba imegundua hazina ya zaidi ya kilomita za mraba bilioni 100 za madini hayo ya helium katika nchi ya Tanzania. Hazina hiyo ni mara 6 zaidi ya mahitaji ya soko la ulimwengu. Tanzania kama nchi nyingine za ulimwengu wa 3 zina rasilimali nyingi ambazo zingeweza kuwasaidia wakazi wake, lakini kinyume chake wakazi wa nchi hizo wanaogelea katika dimbwi la umasikini. Haitashangaza ugunduzi wa gesi hiyo kuendelea kutowasaidia chochote kama ilivyo kwa madini mengine na pia gesi ya Mtwara ambayo haioneshi faida japo kwa wanamtwara.

Gazeti la ***THE EAST AFRICAN*** Katika chapisho la wiki ya tarehe aprili 15 mpaka 21 rais wa Sudan kusini Salva Kiir alisaini mkataba wenye utata. Mkataba huo wa mafuta umesainiwa katika kipindi cha chini ya miezi 4. Wasomi kadhaa wamesema kwamba mkataba huo ni feki na utaiingiza nchi hiyo katika matatizo zaidi ya kiuchumi. Umesainiwa haraka kama namna ya nchi kujikwamua kutoka katika tatizo la ukosefu mkubwa wa fedha.

Nchi 'changa' kama Tanzania leo hii zinajikuta haziwezi kunufaika na utajiri wa madini na rasilimali mbalimbali kutokana na mikataba ya kinyonyaji ambayo husainishwa na kampuni za mabepari wa kimagharibi. Viongozi wengi wanajikuta wanalazimika kusaini mikataba hiyo ya kidhulma kwa sababu kunakuwa hakuna nchi yenye mfumo mbadala ambapo wanaweza kuingia nao mkataba wa uwekezaji. Wakati wa vita baridi baadhi ya nchi changa zilikuwa zinaingia mikataba na iliyokuwa dola ya kisovieti ya kirusi chini ya ujamaa,na hii ni kwa kuwa dola hii ilikuwa inawapa kidogo maslahi na hivyo kuonekanwa kuwa ni mbadala(japo nao sio mfumo sahihi) ambao ulikuwa unawapa changamoto makampuni ya kibepari ya kimagharibi. Kwa mfano nchi ya Cuba ilikuwa inauza bidhaa zake kwa dola ya kisovieti na kupata faida mara mbili zaidi.

Kwa hakika baada ya kuanguka kwa mfumo wa kijamaa kiulimwengu kuliacha pengo katika siasa za kimataifa. Pengo hilo limezifanya nchi za kimagharibi kuendelea kuzikoloni dola za kiafrika bila ya upinzani wa kimfumo kama wakati kulipo kuwepo na ujamaa; wahuni wawili waliokuwa wakivutana kukoloni. Leo hii madola ya kimagharibi yananyonya rasilimali za umma ambazo zinapatikana katika bara la Afrika na kote ulimwenguni kusiko na nchi za kimfumo.

Bara la Afrika, kama ilivyo kwa ulimwengu wote, linahitaji kupatikane mfumo mbadala wa ubepari ili lipate nafuu na kuondokana na unyonywaji wa madola ya kimagharibi ambayo ni ya kibepari. Ni Uislamu pekee unaotosheleza kuwa mfumo mbadala kwa ulimwengu wa sasa. Dola ya kiislamu khilafah ambayo ndiyo itakuwa inabeba ulinganizi wa kiislamu inatosha kuwa ni dola mbadala ya kufanya uchumi na sekta nyingine zote za maisha ulimwenguni.

**Kwanza** dola ya kiislamu khilafah itakuwa inafanya biashara na biladi za kiafrika na hili litasaidia kuziinua kiuchumi dola hizi na biladi za kiafrika zitaacha kufanya biashara na madola ya kimagharibi

.**Pili** dola ya kiislamu itabadilisha mfumo mzima wa usimamizi na usambazwaji wa rasilimali katika biladi ambazo zitakuwa zinasimamiwa na dola ya khilafah.

Rasilimali hizi za gesi na madini kwa mujibu wa uislamu ni milki za ummah na kuwamilikisha watu binafsi ni kuusaliti ummah na kuutia ummah kwenye dimbwi la umasikini kwa kuwadhulumu haki zao. Na rasilimali za ummah pia ni mali za kijamii ambapo haifai mtu binafsi kunufaika nazo peke yake.

Dalili ya hili hupatikana katika hadithi ya mtume Muhammad (saw) iliyopokelewa kutoka kwa abi kharash na baadhi ya maswahaba ambapo mtume (saw) anasema kwamba ***"………watu ni washirika katika mambo 3 ambayo ni maji, malisho na moto"*** kwa hiyo kwa mujibui wa hadithi hii ni kwamba uislamu umeweka wazi kwamba vyanzo vyote vya maji ni milki ya jumuiya yaani mtu binafsi haruhusiwi kumiliki yaani kwa maana pana ni kwamba vyanzo vyote vya maji iwe ni mito, bahari, maziwa, visima hairuhusiwi mtu binafsi kumiliki peke yake bila ya ummah kunufaika nazo. Katika nukta ya vyanzo vya moto kwa muktadha wa sasa unalenga kutoruhusu vyanzo vyote vya nishati kumulikishwa mtu binafsi vyanzo hivyo ima viwe ni gesi, mafuta, umeme na kadhalika.

Hakika ulimwengu huu Bila Khilafah ni utumwa na dhulma.

**Na;**

**Kaema Juma**

# Fikra hatari za kuuangamiza uislam na Kuuimarisha Umagharibi

## Katika Lulu za Hizb-ut-Tahrir

### UKURUBA BAINA YA DINI MBALIMBALI

Katika kitabu kilicho andikwa na kuchapwa na Hizb-ut-Tahrir kikiwa miongoni mwa vitabu vya ziada na kidogo sana kwa jina la FIKRA HATARI ZA KUUSHAMBULIA UISLAM NA KUIMARISHA UMAGHARIBI tunapata ufaham huu;

Kuwalingania watu wasiokuwa waislam ili waingie katika uislam ni jambo la wajibu kwa kila muislam na waislam. Waislam wamekuwa katika wajibu huu kwa zaidi ya karne 14 waki walingania watu wote ima wakitabu au wasiokuwa wakitabu kuingia kataika uislam. Kwakuwa Mwenyezi Mungu SW Anasema;

ادْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

(النحل: 125)

Waite (watu) waelekee kwenye Njia ya Mola Wako Mlezi kwa hekma na mawaidha mema na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (TMQ, An-nahl 125)

Naye Mtume SAW katika barua yake kwa Mfalme Roma Anasema "**hakika nina kulingania kwa ulinganizi wa kiislam. Silimu utasalimika na Allah SW Atakulipa mara mbili. Kama utapinga dhambi utabeba madhambi ya watu walio katika utawala wako.**"

Kwa maana hiyo, Da'awah yetu (waislam) kwa wasiokuwa waislam ni kuwalingania kuukubali Uislam na kujitenga na Ukafiri.

Hii fikra ya Dini Mseto inayo sambazwa hivi leo ni ngeni, ovu na ni fikra ya kimagharibi na kamwe haina msingi wowote wa dalili kuchimbukia katika uislam. hii ni kwa sababu inalingania ukuruba baina ya dini/aqidah tofauti. Inalingania katika Dini mpya iliyo undwa na kuwataka waislam washikamame nayo badala ya Uislam kwa sababu waasisi na wapigia debe fikra hii ni wenyewe makafiri.

Fikra hii ilianza rasmi mwaka 1932 ambapo Ufaransa ilituma wawakilishi wake katika Chuo kikuu cha Misri Al-Azhar ilikujadili namna ya kuunganisha imani kuu tatu, yaani Uislam, Ukristo na Uyahudi.

Mwaka 1964 Papa Paulo wa VI aliandika barua kwa ajili ya wito wa majadiliano baina ya dini mbalimbali. Kisha Vatican (makao makuu ya Kanisa la Roma) yaka chapisha kitabu mwaka 1969 kikiwa na jina la ***Muongozo kuelekea majadiliano baina ya Waislam na Wakristo.***

ilipofika miaka ya 1990 ndipo walingania fikra ya dini mseto walianza kuchangamka zaidi. Likafanyaika kongamano kubwa la Waarabu-Wazungu mwaka 1993 nchini Jordan kisha Sudan mwaka 1994 na likafuatia la mwaka 1996 kwajina la **Uislam na Ulaya** lililofanyika katika Chuo kikuu cha Ahl al-Bayt Jordan.

**Badhi ya Maazimio ya Kongamano:**

1.Kuyarejea na kuunda ufahamu mpya wa maneno kama Kafir, Mshirikina, Muumin, Uislam, Ukatikati, Siasakali na kuhakikisha maneno haya hayawi sababu ya kuwatenganisha watu.

2.Kubainisha mambo yajumla kwa imani hizi tatu ikiwa ni pamoja na Imani, maadili, utamaduni na kuhamasisha ushirikiano chanya kwakuwa watu wote wamekubaliana wana muamini na kumuabudu Mungu.

Kuandaa andiko la pamoja linalo elezea ufahamu mmoja wa haki za binadam . Itaondoa hisia za utofauti wa damu baina ya wanadini na utofauti wa tamaduni za watu wa dini tofauti.

Kufanya mabadiliko ya mitaala ya elimu na historia ili kusiwepo na chochote cha kuonesha utofauti baina ya dini hizi. Kusitishwe baadhi ya masomo ya dini yanayo onesha utofauti wa dini hizi.

Kuamsha raghba ya watu kusoma masomo yafuatayo yakiwa yamejengwa kwa ufahamu mmoja; Usawa, amani, haki za wanawake, haki za binadam, demokrasia, uhuru, amani ya dunia, jumuiya za kiraia, nk.

***Kitaendelea Toleo Lijalo***

## MEI MOSI

*Inatoka Uk 5*

Mfano mmoja katika mingi ni zama za Utawala wa kiislam chini ya Mtume saw, ambapo Ansar mmoja alimwendea Mtume SAW ,akamuomba (amkidhie shida zake). Mtume SAW akamuuliza: Je, una chochote nyumbani kwako? Akajibu: Ndiyo, nina kipande cha nguo, sehemu ya nguo hiyo tuna vaa na sehemu tuna tandika chini, na bakuli ya mti tunayo nywea maji. Akasema SAW: Kavilete hapa. Basi Ansar akavipeleka kwa Mtume SAW vitu vile. Basi Mtume SAW akavipokea na kuvishika, akavinyanyua na kuuliza; ninani atanunua vitu hivi?. Akajitokeza mtu mmoja akasema; najitolea kuvinunua kwa dirham moja. Mtume SAW akarudia mara mbili au tatu ; ni nani atavinunua kwa gharama ya zaidi ya dirham moja?. Mtu mwingine akasema, mimi nitavinunua kwa dirham mbili. Basi Mtume SAW akachukua zile dirham na kumkabidhi Yule mwenye shida na vitu akamkabidhi aliye nunua. Kisha Akamwambia ansar: dirham moja nunulia chakula kwa ajili ya familia yako na dirham yapili nunu shoka kisha uvilete hapa. Basi ansar akaenda kunua na akamletea Mtume SAW ambaye kwa mkono wake alitia mpini katika shoka lile. Akamuagiza ansar Yule kwamba; nenda kakusanye kuni kisha uuze, na usije kuniona kabla ya wiki mbili. Basi Yule mtu aliondoka nakwenda kukusanya kuni na kuuza. Alipo fikisha dirham kumi alikuja kwa Mtume SAW akamwambia, nimenunua nguo na chakula kwa sehemu ya dirham (alizo pata) (Imepokewa na Abu Dawd, hadith namba 1637). Katika urasilimali niwafanywakazi na sio wafanyakazi.

Bila ya khilafah ni Utumwa na Dhulma.

**Na:**

**Abuu Nusaybah**



# BILA KHILAFAH:

# DAMU YA WAISLAM NI DAMU YA MAJARIBIO YA SILAHA:

Mnamo tarehe 23.04.2017 Marekani ili shambulia jimbo la Nangarhar, mashariki mwa Afghanistan. Ilitumia bomu jipya na kubwa kuliko yote duniani likiitwa GBU-43 kufanya uharibifu na udhalilishaji huu kwa kisingizio cha kuwa piga wapiganaji wa Islamic State. Likikadiriwa kuwa na tani 11 za TNT, bomu hilo limesababisha maafa makubwa ndani ya mji huu kwa kupoteza roho za watu na kuharibu mali. wameuwawa wake kwa waume, watoto kwa wazee. www.bbcswahili.com.



Kwa masikitiko makubwa miji mitukufu ya umma wa kiislam leo hii imegeuzwa na tawala khabith za kikafiri kuwa ndio maeneo ya kujaribia silaha zao mpya ama kongwe zilizoboreshwa kitaalamu katika miji yetu.

Thamani na heshima ya miji pamoja na damu zetu leo vimekua duni mbele ya macho ya makafiri kiasi cha kugeuzwa kuwa sehem muafaka na za kimkakati kufanya majaribio ya silaha zao kali za sumu na za kiatomiki, na mara nyengine hata za nyuklia pia.

Hii ni hali mbaya mno ilo ufika umma wetu leo hii baada ya kukosa mtetezi wa maonevu haya yanayofanywa wakati mwingine kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi katika biladi zetu.

Bomu hili linadhihirisha uadui wa kiasi gani wa makafiri katika kuangamiza biladi za kiislam kwani zaidi ya vifo vilivyotokea bado madhra ni endelevu kutokana na uharibifu wa mazingira na uwepo wa gesi chafu na ya sumu iliyo sambazwa na bomu hilo.

Madhara haya kwa mujibu wa wataalam na watafiti mbali mbali wa masuala ya mazingira na hali ya hewa huchukua muda mrefu eneo hili kuwa salama na kurudi katika hali yake ya kawaida ya kuwa ni sehem salama kwa makaazi ya maisha ya watu kwa mara nyingine.

Swali muhimu la kujiuliza kutokana na tukio hili na mengi kama haya yanayofanywa na madola ya kikafiri kila siku katika miji ya kiislam kama vile Iraq, Yemen, Syria, Somalia, Nigeria na mengineyo ambayo msururu wa idadi yake ni mrefu mno na unawozidi kila uchao leo hii, ni waislam wangapi wameshauwawa na wengine kupata ulemavu wa kudumu kutokana na jinai hizi mbaya katika miji yao ?

Na ni athari za kiasi gani zimebaki katika mazingira na hali ya hewa ya miji hii ya kiislam inayosimamiwa na vibaraka duni wasiojali thamani ya damu za waislam na kuiacha imwagwe kiholela na mabwana zao wa kimagharibi.

Mwisho tuna malizia kwa kusema thamani na heshima ya damu na biladi za kiislam kamwe hazitoweza kuhifadhika chini ya usimaizi wa viongozi vibaraka walioko leo hii bali ni kufanya kazi na kuirejesha dola ya kiislam ya khilafa kwa njia ya utume. Na kufanya hivi ndio njia pekee itakayodhamini hadhi na kuzinusuru damu na biladi zote za kiislam.

Qur'an 24:55

"….Atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao…".

**Na SULEIMAN KHAMIS.**

# SWALI KWA AMIRI

# ZAKA YA DENI







**Swali:**
Assalamu Alaikum wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

Mimi ni mfanyakazi katika moja ya Vyuo Vikuu vya Palestina na maranyingi ninafanya kazi mpaka muda wa ziada (overtime) na kawaida huwa hatulipwi malipo ya muda wa-ziada kwa wakati bali chuo hutuwekea kama deni kwa kulilimbikiza, na huenda deni la mmoja wetu lika zidi kiwango cha *Nisab* (baada ya kupitikiwa na mwaka). Hili deni lina uhakika wakulipwa ila tu muda wakulipwa ndio haujulikani. Kwamfano, kwa miaka mine sasa sijawahi kulipwa malipo hayo ya muda wa ziada, na wala sifahamu kwamba nilini nitalipwa. Je, kwa pesa hizi ninazo dai kuna kulipia zaka?. Na iwapo kuna Zakat, je, inalipwa kwa maramoja nitakapo lipwa au nikwa kila mwaka?. Fahamu kwamba wengi wa sisi wahadhiri jambo hili lina tuchanganya sana hivyo tunatafuta kujua hukmu sahihi. Mwenyezi Mungu akulipe.

**Jibu:**
Wa Alaikum Assalam wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

**Nimefahamu kutoka katika swali lako kwamba malipo hayo ya overtime (muda wa ziada) ni makubaliano ya kmkataba na Chuo Kikuu, kwamba kwa kazi hii unastahili malipo maalum pindi unapo maliza kazi hizo, na iwapo hawakukulipa kwa wakati malipo hayo hubakia kuwa ni deni kwao…** wala sio bakhshishi (bonus) au nyongeza kwa kujitolea kufanya kazi za ziada ambapo ingewapasa kukulipa kiasi wanachotaka pindi watakapo taka, yaani ima kingi au kichache, au hata wasikupe chochote… iwapo ufahamu wangu ni sahihi wa hayo maelezo yako, basi jawabu la swali lako lipo wazi katika kitabu *Mali katika Dola ya Khilafah (Al-Amwal fi Dawlat Al-Khilafah)* kwa maelezo haya:

(… Ikiwa mtu ana anadeni (anadai) kwa mtu tajiri ambaye anaweza kumlipa muda wowote, ni wajibu kwake kulipa Zakat ya lile deni linapo pitikiwa na mwaka. Amesimulia Ibn Ubaid ra kutoka kwa Umar ibn Al-Khatwab ra kwamba "Inapofika saqah kuwa wajibu, hesabu madeni yako na ulicho nacho kuwa ni kitu kimoja (kwa pamoja) kisha tolea Zakat". Uthman Ibn Affan amesema: "Sadaqah ni wajibu kwa deni ambalo unaweza kulipata kutoka kwa mdaiwa unapohitaji, na deni ambalo lipo kwa mtu anaye chelewesha kulilipa na wewe unaliacha kwa kuona haya au kama zawadi (favour) ; ni Sadaqah". Amesimulia Abu Ubeid, ambaye pia amepokea kutoka kwa Ibn 'Umar amesema: "Katika kila madeni yako ambayo unataraji utalipwa niwajibu kuyatolea Zakat pindi yakizungukiwa na mwaka."

Aidha iwapo deni lipo kwa mtu masikini ambaye yupo katika mazingira magumu, au kwa tajiri anaye lizuia (kulipa deni hilo), basi sio wajibu kwa mdai kulipa Zakat mpaka atakapo lipwa (denilake). Na baada ya kulipwa atatoa chote kilicho wajibika kutolewa kwa miaka yote. Ila kuhusu deni lenye mashaka, mfano mdai hana uhakika kwamba atalipwa aua laa, Ali ra anasema: "Ikiwa ni muungwana basi alipe Zakat mara tu atakapo lipwa deni lake kwa hicho kipindi." Imesimuliwa na Abu Ubeid, ambaye pia amesimulia kutoka kwa Ibn Abbas amesema kuhusu madeni kwamba: "Iwapo huna uhakika wa kulipwa (denilako), usililipie Zakat yake mpaka pale utakapo lipwa. Pindi utakapo lipwa lipa kile kinacho liwajibikia (hilo deni)." Mwisho wa yaliyo elezwa katika kitabu cha *Mali katika Dola ya Khilafah (Al-Amwual fi Dawlat Al-Khilafah)*

Hivyohivyo, malipo yako ambayo yanashikiliwa na Chuo kikuu kama denilako kwao, Zakat kwa malipo haya sio lazima kufanyika sasa hivi, lakini ni wajibu kulipwa Zakat mara tu utakapo pokea malipo yako kutoka kwa Chuo Kikuu kwa sababu hufahamu ni lini utalipwa.

Hii nikwamba deni lako huwezi kulihitaji kutoka kwa Chuo Kikuu na kulipata kwa muda unaohitaji. Kwahali hii basi, Zakat kwa pesa hizi inakuwa ni wajib kwako mara tu utakapo zipata na kwa wakati huo, kisha utazitolea Zakat kwa miaka iliyopita kuanzia pale ambapo fedha zako zilifikia *Nisab* na kisha kupitiwa na mwaka. Kwahiyo ni wajibu kulipa Zakat kwa miaka yote baada ya mwaka kupita kwamali/pesa ambayo imefikia kiwango cha *Nisab,* nawala sio kuilipia Zakat yake kwa mwaka mmoja , ila nikwa miaka yota baada ya *Nisab* kutimia na kupitiwa na mwaka……

Nina Muomba Allah SW Akujaalie Baraka katika fedha zako, familia na watoto wako.

**Ndugu yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**
*Imewekwa katika Kiswahili*

***Na: Hamza Sheshe***

# ISTILAHI YA “AHLUSU

**Sehemu y**

## SUNA KUELE

Na: Abu Malik Thair Salama

Kwa Ofisi kuu ya I

Na jambo la pili la kuzingatia ni kauli ya Mtume ( S.a.w ) katika Hadithi Mashuhuri ambayo kaipokea Imam Muslim na wengineo kwa Hadithi ya Jariri bin Abdillah Albjli ( Radhiallah Anhu) amesema :

في الحديث المشهور الذي أخرجه الإمام مسلم وغيره من حديث جرير بن عبد الله البجلي رضي الله عنه قال: قال رسول اللهr: «مَنْ سَنَّ في الإسْلام سُنةً حَسنةً فَلَهُ أَجْرُهَا، وأَجْرُ منْ عَملَ بِهَا مِنْ بَعْدِهِ مِنْ غَيْرِ أَنْ ينْقُصَ مِنْ أُجُورهِمْ شَيءٌ، ومَنْ سَنَّ في الإِسْلامِ سُنَّةً سيِّئَةً كَانَ عَليه وِزْرها وَوِزرُ مَنْ عَمِلَ بِهَا مِنْ بعْده مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أَوْزارهمْ شَيْءٌ».

Amesema Mtume ( S.a.w ) “Mwenye Kuendeleza katika Uislam Mwenendo Mzuri atapata Malipo yake na Malipo Mwenye Kuufanyia kazi Mwenendo huo baada yake,pasina kupungua chochote katika Malipo yao,na Mwenye kuendeleza Mwenendo Mbaya katika Uislam,atapata Madhambi na madhambi ya wale watakaoufanya Baada yake ,pasina kupungukiwa na chochote katika Madhambi yao”

Hapa amehesabu Mtume (S.a.w ) Mwenendo (Sunnah) Mzuri na unaelekeana na Uzushi (Bid’a) ambao unamtoa nje ya Njia mwenye kuufanya,ili umtupe katika Maporomoko ya Bid’a ( Uzushi ) yaani kutoka katika njia ya Kisunnah yaani Mwenendo au Njia ambayo aliwaachia Mtume ( S.a.w ) Waislam,kawaacha katika njia nyeupe usiku wake kama mchana wake hatokwenda kando nao isipokuwa ataangamia,na atapotea,na mkusanyiko wa sunnah hizi nzuri ndio njia ya Uislam katika Maisha ambayo katuamrisha Mtume (S.a.w) Kushikamana nayo na tuing’ate kwa Magego na kushikamana na yote yaliomo humo.

Umekuja Uislam Ukiwa ni Mfumo kamili wa Maisha,Mwenye Kutoka Nje yake atakuwa amefanya Uzushi na mwenye kufanya Uzushi atapotea :

Hadithi hii :

«مَنْ سَنَّ في الإِسْلام سُنةً حَسنةً»

“Mwenye Kuendeleza katika Uislam Mwenendo Mzuri atapata Malipo yake na Malipo Mwenye Kuufanyia kazi Mwenendo huo baada yake,pasina kupungua chochote katika Malipo yao……” hii ina maana ya kuwa mwenye Kufungua njia ya sunnah ya kisheria(1) hii kwa sababu kule kuwa Sunnah Ni Nzuri au Mbaya haiwezekani kulifahamu hilo isipokuwa kwa Njia ya Sheria,na wala kwa njia ya kiakili,haitakikani kwa Mwanaadamu yoyote mwenye punje ya Imani aseme kitu ni kizuri au ni kibaya kwa kutumia akili yake,Yaani Kwamba Sunnah katika Lugha ya Sheria inakusanya Hukmu zote za Kisheria,hiyo ndio njia ambayo kaipitia Mtume wetu ( S.a.w ) na Mgawanyo na upambanuzi wake unafahamika katika Dalili za Kitabu na Sunnah.

Kwenye utangulizi wa kitabu cha Sunanid Daarimy :

وفي سنن الدارمي كتاب المقدمة: عن أبي عبد الرحمن قال: قال عبد الله: "اتبعوا ولا تبتدعوا فقد كفيتم".

Toka kwa Abdurrahmani amesema : Amesema Abdullah : Fuateni na Wala Msizushe kwa hakika Mmeshatoshelezwa” Kufuata ina maana kwamba hakuna Mashaka kuishi kwa Mujibu wa njia Maalum ambayo usiku wake ni Mweume kama Mchana wake.

Kutokana na haya imekuwa ni kawaida kufahamika Ibnu Sirin Allah amrehemu kwamba watu imma watakuwa Ahlu sunnah ,na Imma watu wa Bid’a ,yeye ni mtu wa Mwanzo ambaye limepokelewa katika Maneno yake neno “Ahlu sunnah kwa kuelekeana na Ahlul Bid’a” na wala hakuwa akikusudia kukisifika kikundi katika vikundi vya Waislam kwa kuelekeana na kikundi kingine kama Mu’utazila na Jebria,kwani katika wakati wake ilikuwa bado ufahamu haujaharibika,na bila shaka alichukuwa kwenye hadithi kwamba ima uisimamishe Sunnah au uifanyie kazi Bid’a.!

Kuhuisha Sunnah : Ni Kuifanyia Kazi na Kuitekeleza Kivitendo

Toka kwa Kathir bin Abdillah toka kwa Baba yake,amesema toka kwa Babu yake kwamba Mtume (S.a.w) alimwambia bilali Bin Harithi : Fahamu Ewe Bilali ,Akasema :

قال لبلال rعن كثير بن عبد الله عن أبيه عن جده أن النبي قَالَ: مَا أَعْلَمُ يَا رَسُولَ اللهِ؟ قَالَ: «اعْلَمْ!»بن الحارث: أَنَّهُ مَنْ »قَالَ: مَا أَعْلَمُ يَا رَسُولَ اللهِ؟ قَالَ: «اعْلَمْ يَا بِلَالُ!» أَحْيَا سُنَّةً مِنْ سُنَّتِي قَدْ أُمِيتَتْ بَعْدِي فَإِنَّ لَهُ مِنَ الأَجْرِ مِثْلَ مَنْ عَمِلَ بِهَا مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أُجُورِهِمْ شَيْئًا وَمَنِ ابْتَدَعَ بِدْعَةً ضَلاَلَةٍ لاَ يَرْضَاهَا اللَّهُ وَرَسُولُهُ كَانَ عَلَيْهِ مِثْلُ آثَامِ مَنْ عَمِلَ بِهَا لاَ يَنْقُصُ ذَلِكَ مِنْ أَوْزَارِ النَّاسِ شَيْئًا».

“Nifahamu Nifahamu Kipi ewe Mjumbe wa Allah ? ,Akasema : Nifahamu Nifahamu Kipi ewe Mjumbe wa Allah ? Akasema : Mwenye Kuhuisha Sunnah katika sunna zangu ambao ilikuwa imeuawa baada yangu,kwa hakika atapata malipo mfano wa wale watakaoiteleza pasina kupungua chochote katika malipo yao,na atakaezusha Uzushi wa upotevu ambao Allah hauridhii na wala Mtume wake,atapata Madhambi mfano wa wale wanaoutekeleza na wala hakitapungua chochote kile katika madhambi yao.”

قال أبو عيسى هذا حديث حسن، سنن الترمذي، وابن ماجه، وقال السندي في شرح سنن ابن ماجه: قيل: المراد بالسنة من الأحكام، وهي قد تكون فرضاrهنا ما وضعه رسول الله كزكاة الفطر وغير فرض كصلاة العيد وصلاة الجماعة وقراءة القرآن من غير الصلاة وتحصيل العلم ونحو ذلك، وإحياؤها أن يعمل بها ويحرض الناس ويحثهم على إقامتها.

Amesema Abu Issa Hadithi hii ni Hassan,Sunani Tirmidhi na Ibnu Maajah,na amesema Sindi katika Sharhi ya Sunani Ibn Maajah : Imesemwa : Makusudio ya Sunnah Hapa ni yale alioyaweka Mtume (S.awa) katika hukmu,na huenda zikawa ni Faradhi kama zakatul Fitri na nyingine si za Faradhi kama vile swala ya Iddi na swala ya Jamaa na kusoma Qur’an wakati ukiwa nje ya swala na kutafuta elimu na mfano wa hayo,Kuhuisha kwake ni kuitekeleza na kuhimiza watu waitekeleze kivitendo.

Na amepokea Muslim toka kwa Said Bin Musayyib amaesema : amesema Anasi Bin Maaliki : Kaniambia Mimi Mtume ( S.a.w) :

وروى الترمذي عن سعيد بن المسيب قال: قال أنس بن مالك: قال لي رسول اللهr: « يَا بُنَيَّ، إِنْ قَدَرْتَ أَنْ تُصْبِحَ وَتُمْسِيَ لَيْسَ فِي قَلْبِكَ غِشٌّ لِأَحَدٍ فَافْعَلْ» ثُمَّ قَالَ لِي: «يَا بُنَيَّ وَذَلِكَ مِنْ سُنَّتِي، وَمَنْ أَحْيَا سُنَّتِي فَقَدْ أَحَبَّنِي، وَمَنْ أَحَبَّنِي كَانَ مَعِي فِي الجَنَّةِ».

( Ewe Mwanangu,Ikiwa utaweza kupambazukiwa na kuchwewa na Jua na wala hakuna katika moyo wako Hadaa (Ghishi ) kwa yeyote Basi kuwa hivyo)kisha akaniambia : ( Ewe Mwanangu na kufanya hivyo ni katika sunna zangu,na mwenye kuhuisha Sunna yangu kwa hakika amenipenda na mwenye kunipenda atakuwa nami peponi )

UNNAH WALJAMAA'

ya Tatu

# KEANA NA BID'A

Habari ya Hizb-ut-Tahrir

Na hadithi hii ina kisa kirefu,amesema Abu Issa Hadithi hii ni Hasan Gharibu kwa Upande huu,na imetokea katika baadhi ya Kopi cha Tirmidhi :

«فَقَدْ أَحْيَانِي وَمَنْ أَحْيَانِي».

( Kwa hakika atakuwa amenihuisha mimi na mwenye kunihuisha ..)

وفي أول مسند الكوفيين روى الإمام أحمد عن البراء بن عازب «أَنَّ النَّبِيَّ r رَجَمَ يَهُودِيًّا، وَقَالَ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَشْهَدُكَ أَنِّي أَوَّلُ مَنْ أَحْيَا سُنَّةً قَدْ أَمَاتُوهَا».

Na Mwanzoni mwa Musnad wa Watu wa Kufa kapokea Imam Ahmad toka kwa Albarrau bin Aazib kwamba Mtume ( S.a.w) Alimrujumu Myahudi ,na akasema Mara baada ya tukio hilo " Ewe Mwenyezi Mungu ,Hakika mimi Nakiushuhudisha kuwa ni mimi ni wa Mwanzo kuhuisha sunnah ambayo waliifisha "

Kuhuisha Sunnah ni Kuikeleza Kivitendo na kuifanya ndio Mfumo wa Maisha.

Kutokana na haya Sunnah katika Uislam : Ni njia ya maisha ya Kiislaam,Kunyenyekea Uislam na hukmu zake na kuufanya ndio njia ya Maisha,Mwenye kuhuisha sunna zangu,yaani mwenye kuhuisha njia ya Maisha ambayo nimewachorea Waislam,na ndio mfumo ambao ameuchagua Allah subhaanahu wata'ala kwenu ninyi, ili muishi juu ya msingi wake,ili kudhibiti mahusiano yenu na nafsi zenu na pamoja na watu wengine na Mahusiano yenu na Allah Subhaanahu wataa'lah juu ya msingi huo,basi hicho ndio kiongozi chenu cha kifikra,ambacho mnawajibika kukibeba na kuulingani Ulimwengu juu ya hicho, na ndio msingi wenu wa Kifikra ambao hujengeka juu yake fikra zote na njia zote,yaani kubainisha namna ya kutekeleza tiba na suluhisho ambayo imewekwa na Sheria kutatua matatizo ya Mwanaadamu,na kubainisha namna ya kuihifadhi na kuilinda Itikadi,na kubainisha namna ya kuibeba Da'wah ya Mfumo huu wa kiislaam,Na Msingi huu wa Kifikra vile vile ndio ambao Huchipukia na kuchomozea humo na Juu ya Msingi wake Masuluhisho yote ya Matatizo yote ya Maisha,na Msingi wake huwa ni Maalum katika Muelekeo waKifikra kwa Mwanaadamu na namna ya Mtazamo wake katika Maisha.

Amesema Zamakhashari : Mwenye Kuweka sunna nzuri : Kaweka Njia Nzuri ,na Ukisema Fulani Mwenye Kufata sunnah yaani anaitekeleza Kivitendo .

Na amesema Aljurjaanii : Sunnah katika Lugha ni Njia sawa ni yenye kuridhiwa au isioridhiwa,na kisheria Ni Njia yenye kupitwa na kufuatwa katika Dini pasina ulazima wala uwajibu"

وقال الشريف الجرجاني: "السنة في اللغة الطريقة مرضية كانت أو غير مرضية، وفي الشريعة هي الطريقة المسلوكة في الدين من غير افتراض ولا وجوب"،

Inabinika kutokana na yaliotajwa kuwa sunna katika asili ya matumizi ya kilugha ni Mwenendo na Njia kwa kukusanya maana ya kufuata na kuiga,na katika matumizi ya sheria ni kile kilipendekezwa na Sheria kukifanya kwa namna ya kupendezeshwa na wala si kwa namna ya wajibu,na pia ni yale yaliotoka kwa Mtume (S.a.w) katika kauli zake au vitendo na sifa zake,na ni msingi na asili katika misingi ya Sheria na ni njia ya Maisha ya Kiislam,yaani namna ambayo aliitekeleza Mtume ( S.a.w) na maana zote hizo zina maana ya kujilazimisha kufuata, kwa dalili ya viwakilishi vingi vya maneno ikiwa kumuelezea anaetoka na kuacha sunnah kuwa ni Mzushi.

Jamaa:

Amesema Alkhalil Bin Ahmad katika Kamusi la Al-ain: Al-Jam'u ni Masdar (Chanzo - Asili ) Jama'atus Shay'a na Al-Jam'u : Ni Jina la Kundi la watu,na Jamaa Ni wingi wa kila kitu wingi wake.

Na Amesema Ibnu Duraid : Na Jam'u ni Kinyume cha Kutofatiana,(Khilafu Tafriiq) Jamaatush-Shay'a Ajmauhu Jam'an Nimekikusanya kitu nakikusanya kukusanya,pindi nikikusanya baadhi yake kwa baadhi, na pia pori ni mahala wanapokusanyika watu na wala hawatengani kwa kuogopa kupotea .



Amesema Ibnu Faaris : Jama'a: Jiim na Miim na Ain ni asili moja yenye maana ya Kukusanya kitu.

Amesema Arraghibu Al-Usfahaan : Al-Jam'u dhammuush Shay'in,Jam'u ni kukusanya kitu Baadhi yake kwa baadhi,na husemwa kwa mkusanyiko Jam'u,Jamiiu na Jamaa,Mkusanyikao na mkusanyiko kwa watu waliotawanyika Ijtamauu yaani wamekusanyika.

Na hitimisho la Ufafanuzi huu wa Kilugha unaonyesha kuwa Jamaa ni nina la kundi la watu walioungana na kushikamana na kukurubiana katika Rai.

Angalia :

Kwa mfano : Sadaka ni katika suna za kiislaam za kisheria,Mwenye kufungua njia nzuri ya kuhuisha sunna ya sadaka,kama vile akabuni njia mpya inayopelekea kutekelezwa sadaka,basi atapata malipo kwa kubuni njia hii mpya,kama vile mtu wa mwanzo kufungua mlango wa kuweka maji njiani ili watu wanywe ni njia ya sadaka,basi mwenye kuweka njia ya sadaka na akabuni njia mpya atapata malipo ya watakaotekeleza hilo mpaka siku ya kiama.

Asaasul Balaagha cha Zamakhshari Uk 310

Ataarifaat cha Jurjaani Uk 134

Ahlusunnah wal- Jamaa cha Dr Ahmad Zaqqaqi

Ahlusunnah wal – Jamaa- adhiyaau

Muujamu Mufradatul-Qur'aan Uk 94-95 cha Arraghibu Al-usfuhan.

Maqaayisu Lugha 1/479 cha Ibn Faaris

Muujamu-Ain 1/239-240 cha Khalil Bin Ahmad

Jaamharatul – Lughat 2/103 cha Ibnu Duraid.

***Imetafsiriwa kwa Kiswahili na***

***Sheikh Mussa Kileo***

***Usikose Sehemu ya Nne katika Toleo Lijalo.***




**WANASIASA WA KIISLAM WA HIZB UT-TAHRIR TANZANIAWAKIWA KATIKA AMALI MBALIMBALI**

**ZA KUUZINDUA UMMAH JUU YA KADHIA NYETI YA KUFANYA JUHUDI ZA KUREJESHA SERIKALI YA KIISLAM, KHILAFAH. NI KATIKA KAMPENI MAALUM YA MWEZI WA RAJAB. MWEZI ULIO ANGUSHWA KHILAFAH, RAJAB 1342AH, MACHI 1924**

Jarida la
**Khilafah**

**UKURASA WA FACEBOOK WA AMIRI WA HIZB UT-TAHRIR**
***Kujiongezea mwamko wa usul ul- fiqhi, siyasa, uchambuzi nk.***
***Tembelea Ukurasa wa facebook wa Amiri wa***
***Hizb ut-Tahrir- Sheikh Ataa bin Khalil Abu Rashtah:***
**https://www.facebook.com/Ata.abualrashtah**

**jkhilafahtz@gmail.com**